RIPOTI YA KIMATAIFA YA AMNESTY INTERNATIONAL

# HUKUMU ZA KIFO NA WATU WALIONYONGWA

# 2023

AMNESTY INTERNATIONAL

**Amnesty International ni vuguvugu la watu milioni 10 ambalo huhamasisha ubinadamu wa kila mmoja wetu na kuendesha kampeni ya kuleta mabadiliko ili kwamba sisi sote tuweze kufurahia haki zetu za binadamu. Dira yetu ni kuwa na dunia ambayo wenye madaraka wanatimiza ahadi zao, wanaheshimu sheria za kimataifa na kuwajibishwa. Hatufungamani na serikali, itikadi ya kisiasa, maslahi ya kiuchumi, au dini yoyote na kwa sehemu kubwa tunafadhiliwa na wanachama wetu na michango ya watu binafsi. Tunaamini kwamba kwa kufanya kazi kwa mshikamano na kuwapenda watu kila mahali tunaweza kubadilisha jamii zetu kuwa bora zaidi.**

© Amnesty International 2024

Isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo, maudhui yaliyo kwenye taarifa hii yameidhinishwa chini ya leseni ya Creative Commons (uhusishaji, isiyo ya kibiashara, hakuna vinyambuo, ya kimataifa 4.0)
https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/legalcode

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea ukurasa wa idhini kwenye tovuti yetu:
www.amnesty.org

Pale ambapo maandishi yanahusishwa na mmiliki wa hakimiliki ambaye ni tofauti na Amnesty International, maandishi hayo hayatakuwa chini ya leseni ya Creative Commons.

Imechapishwa mara ya kwanza mwaka 2024 na Amnesty International Ltd
Jumba la Peter Benenson, Barabara ya 1 Easton, London WC1X 0DW, Uingereza

**Fahirisi: ACT 50/7952/2024 Kiswahili**
**Lugha asilia: Kiingereza**

**amnesty.org**

AMNESTY INTERNATIONAL

# MATUMIZI YA ADHABU YA KIFO 2023

> ***"Hatuwezi kupuuza kuwepo kwa haki ya kuishi kwa kila binadamu. [...] Hukumu ya kifo haijaleta matokeo ambayo ilinuiwa kuleta"***
>
> Ramkarpal Singh, Naibu wa Waziri katika Idara inayohusika na Sheria na Mageuzi ya Kitaasisi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu[1]

## MIENENDO YA KIMATAIFA

Ufuatilizi wa Amnesty International umeonyesha kwamba mnamo 2023 idadi ndogo zaidi ya nchi kwenye rekodi zinajulikana kwamba ziliwanyonga watu wengi zaidi katika kipindi cha karibu mwongo mmoja. Takwimu hizi zinathibitisha mwenendo wa miaka ya hivi karibuni ambao unaashiria kuendelea kutengwa kwa nchi ambazo zinatoa hukumu ya kifo kwa makosa madogo madogo.

Ongezeko la idadi iliyorekodiwa ya watu walionyongwa lilitokana na kuongezeka pakubwa kwa watu kunyongwa kutokana na makosa yanayohusiana na dawa za kulevya nchini Iran, kuchochewa na mamlaka za nchi hiyo kupuuza kabisa vikwazo vya kimataifa kuhusu matumizi ya adhabu ya kifo. Kando na kwamba makosa haya huenda yasipewe adhabu ya kifo chini ya sheria ya kimataifa, pia adhabu hizi ziliathiri jamii za Iran ambazo zimetengwa sana, hasa wanaume na wanawake kutoka kwa jamii ya wachache ya Baluchi ambayo imekuwa ikinyanyaswa.

Idadi hizi za jumla ambazo zinajulikana zinajumuisha maelfu ya watu wanaoaminika kunyongwa nchini Uchina, ambayo imekuwa ikiongoza duniani kwa kuwanyonga watu; na Korea Kaskazini na Viet Nam, nchi ambazo zinaaminika kuendelea kuwanyonga watu kwa wingi, ingawa hakuna data zilizopo kuonyesha hili.

Usiri na kudhibitiwa kwa taarifa kuhusu adhabu za kifo ni ishara kwamba serikali za baadhi ya nchi zinazoendelea kuwanyonga watu zimejitolea kuendelea kutumia adhabu hii kama nyenzo ya kuwatia watu hofu na kuonyesha nguvu ya taasisi za dola. Takwimu za adhabu ya kifo zilibakia kuwa siri za dola nchini Uchina na Viet Nam. Ingawa kuripoti kuhusu hukumu za kifo na watu walionyongwa ni jambo lililodhibitiwa sana katika nchi hizi mbili na pia nchini Korea Kaskazini, mamlaka kwa njia banifu ziliondoa usiri kwa baadhi ya kesi kama kikumbusho kwamba uhalifu, au ukiukaji wa kanuni zilizowekwa unaweza kuadhibiwa vikali. Nchini Myanmar, mamlaka za kijeshi ziliendelea kutoa hukumu ya kifo katika mahakama zinazodhibitiwa na jeshi, katika kesi zinazoendeshwa kwa usiri na ambazo haki haizingatiwi kamwe. Vivyo hivyo, mamlaka katika baadhi ya majimbo ya Marekani walikuja na miswada ya kudumisha usiri katika kupata vifaa au vitu vitakavyotumika kuwanyonga watu ili kujikinga wasichunguzwe - mfano ni kuhaririwa kwa sehemu kubwa za itifaki mpya ya kuwanyonga watu kwa kutumia gesi ya nitrojeni jimboni Alabama.

---

[1] Al Jazeera, "Bunge la Malaysia linafanya uamuzi kukomesha adhabu ya kifo ", 3 Aprili 2023, aljazeera.com/news/2023/4/3/malaysias-parliament-votes-to-abolish-the-death-penalty

Mjadala wa kuunga mkono adhabu ya kifo ulinoga katika baadhi ya nchi kufuatia visa vya uhalifu wa hali ya juu au kabla ya uchaguzi licha ya kuwa hakuna ushahidi kwamba adhabu hii inaweza kuwazuia watu kutekeleza uhalifu. Kufuatia kesi kadhaa za hadhi ya juu, mnamo Septemba Bunge la Taifa la Korea Kusini lilipitisha mabadiliko ya sheria ili kuweka adhabu ya kifo kama adhabu ya juu zaidi kwa makosa ya mauaji au kuwatupa watoto wachanga waliozaliwa. Nchi kama vile Taiwani na Marekani pia ziliomba watu waadhibiwe kifo kama sehemu ya kampeni za uchaguzi wa urais.


Pingamizi za miaka mingi kutoka kwa nchi kadhaa zikitaka adhabu ya kifo ikomeshwe zilionekana kuzaa matunda mnamo 2023. Katika mwezi wa Julai, kufutiliwa mbali kwa adhabu ya kifo kwa makosa yanayohusiana na dawa za kulevya nchini Pakistan na kukomeshwa kwa adhabu ya kifo ya lazima nchini Malaysia kulianza kutumika; na Bunge la Ghana lilipiga kura kuunga mkono miswada miwili ambayo ingeondoa adhabu ya kifo kutoka kwa kanuni za sheria ya jinai na ya kijeshi.

Mambo haya yalionyesha kwamba ajenda ya haki za binadamu inapowekwa katikati ya mipango ya serikali, inawezekana kufikiria upya kuhusu namna uhalifu unavyoshughulikiwa na kuanza kubadilisha jinsi tunavyotumia rasilmali kutoka kuadhibu na kuangazia kuzuia na kuwarekebisha wahalifu. Nchi nyingi sana duniani tayari zimefanya chaguo hili na kukomesha adhabu ya kifo katika sheria zake au utekelezaji. Kufikia mwisho wa mwaka 2023, miswada ya kuondoa sheria hii katili ilikuwa ikisubiri kupitishwa na mabunge ya Kenya, Liberia na Zimbabwe. Maendeleo haya yalitoa matumaini mapya kwamba siku moja, miaka inavyopita, ulimwengu mzima unaweza kuondokana na adhabu ya kifo.

## IDADI YA WATU WALIONYONGWA

Amnesty International ilirekodi watu 1,153 walionyongwa mnamo mwaka wa 2023, ambalo ni ongezeko la asilimia 31 (270) kutoka watu 883 ambao tunajua kuwa walinyongwa mwaka wa 2022. Ndiyo idadi kubwa zaidi kurekodiwa na Amnesty International tangu idadi ya mwaka wa 2015 ambayo ndiyo iliyokuwa kubwa zaidi; na ni mara ya kwanza tangu 2016 (1,032) ambapo idadi ya jumla inayojulikana ilikuwa zaidi ya 1,000 (*angalia mchoro 1*).

### MCHORO 1: IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA DUNIANI 2014-2023



Idadi hii ya jumla inayojulikana haijumuishi maelfu ya watu ambao wanaaminika kwamba walinyongwa nchini Uchina, ambayo mwaka wa 2023 ilibakia kuongoza duniani kwa kuwanyonga watu.[2] Aidha, Amnesty International haingeweza kubainisha idadi ya chini ya watu walionyongwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea (Korea Kaskazini) na Viet Nam, nchi ambazo zinaaminika kuwa zinaendelea kuwaadhibu watu kifo kwa wingi. Kutokana na hili, idadi ya jumla iliyowekwa kwenye ripoti hii ni ya chini na ambayo inaelezea kwa njia isiyo kamilifu kuhusu nchi zilizogeukia kuwanyonga watu mwaka huo.

### IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA DUNIANI 2023

Afghanistan (+), Bangladesh (5), Uchina (+), Misri (8), Iran (853+), Iraq (16+), Kuwait (5), Korea Kaskazini (+), Palestina (Nchi ya) (+), Saudi Arabia (172), Singapore (5), Somalia (38+), Syria (+), Marekani(24), Viet Nam (+), Yemen (15+).

Ongezeko kubwa la idadi ya jumla ya watu walionyongwa lilitokana hasa na ongezeko la watu walionyongwa nchini Iran (asilimia 48, yaani kutoka watu 576 mnamo 2022; na pia ongezeko la zaidi ya mara mbili, kutoka 314 mnamo 2021). Hili lilishuhudiwa hasa katika visa vilivyohusu kuwanyonga watu waliohusishwa na dawa za kulevya ambao waliongezeka kutoka 255 mnamo 2022 hadi 481 mwaka wa 2023.

Asilimia 74 ya idadi iliyorekodiwa ya watu ambao walinyongwa ilikuwa ya watu kutoka Iran pekee; na asilimia 15 walitoka Saudi Arabia. Nchi hizi mbili zilitoa asilimia 89 ya jumla ya watu wanaojulikana kunyongwa.

Ongezeko la watu walinyongwa pia lilirekodiwa hasa nchini Somalia (kutoka 6+ mnamo 2022 hadi 38+ mnamo 2023, ambalo ni ongezeko la mara sita); Marekani (kutoka 18 mnamo 2022 hadi 24 mnamo 2023, ambalo ni ongezeko la asilimia 33); na Yemen (kutoka 4+ hadi 15+, karibu mara nne ya mwaka uliotangulia).

Inajulikana kwamba wanawake walinyongwa nchini Uchina (+), Iran (24), Saudi Arabia (6), Singapore (1).

Rekodi zinaonyesha kwamba watu walinyongwa katika nchi 16 ambayo ndiyo idadi ya chini zaidi kuwahi kurekodiwa ya nchi zinazowanyonga watu tangu Amnesty International ilipoanza kufuatilia. Hakuna watu waliorekodiwa kuwa walinyongwa nchini Belarus, Japan, Myanmar na Sudan Kusini, nchi ambazo zilizowanyonga watu mnamo 2022 (nchi 20 kwa ujumla).

### NCHI ZINAZOJULIKANA NA MASHIRIKA YA KIMATAIFA KUWA ZILIWANYONGA WATU MWAKA 2023

- Muungano wa Madola ya Amerika: Nchi 1 kati ya 35 ziliwanyonga watu - Marekani
- Shirika la Usalama na Ushirikiano Ulaya Nchi 1 kati ya 57 ziliwanyonga watu - Marekani
- Umoja wa Afrika: Nchi 2 kati ya 55 ziliwanyonga watu - Misri, na Somalia
- Juimuiya ya Nchi za Kiarabu: Nchi 8 kati ya 22 ziliwanyonga watu - Misri, Iraq, Kuwait, Palestina (Nchi ya), Saudi Arabia, Syria, Somalia na Yemen
- Umoja wa Nchi za Asia ya Kusini-Mashariki: Nchi 2 kati ya 10 ziliwanyonga watu - Singapore na Viet Nam
- Jumuiya ya Madola: Nchi 2 kati ya 56 ziliwanyonga watu - Bangladesh na Singapore
- Jumuiya ya Nchi Zinazozungumza Lugha ya Kifaransa: Nchi 2 kati ya 54 ziliwanyonga watu - Misri, na Viet Nam
- Umoja wa Mataifa: Nchi 15 ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (asilimia 8) kati ya 193 zinajulikana kuwa ziliwanyonga watu – Afghanistan, Bangladesh, Uchina, Misri, Iran, Iraq, Kuwait, Korea Kaskazini, Saudi Arabia, Singapore, Syria, Marekani, Viet Nam na Yemen.[3]

---

2 IMnamo mwaka wa 2009, Amnesty International iliacha kuchapisha takwimu za watu waliokadiriwa kupewa adhabu ya kifo Uchina. Badala yake shirika hilo limetia changamoto mamlaka za nchi hiyo kuthibitisha madai yao kwamba wanafanikisha lengo lao la kupunguza matumizi ya adhabu ya kifo kwa kuchapisha takwimu hizo wenyewe. Taarifa kamili au zisizo kamilifu zilipatikana kwa nchi zingine kadhaa (angalia kiambatisho cha Amnesty International kuhusu matumizi ya adhabu ya kifo kwenye ripoti hii kwa taarifa zaidi).

3 Nchi ya Palestina ina hadhi ya Nchi mwangalizi isiyokuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa.


## NJIA ZILIZOTUMIKA KUWANYONGA WATU 2023[4]

| | |
|---|---|
| Kukata kichwa | Saudi Arabia |
| Kutia kitanzi | Bangladesh, Misri, Iran, Iraq, Kuwait, Singapore, Syria |
| Kudunga sindano ya sumu | Uchina, Marekani, Viet Nam |
| Kupiga risasi | Afghanistan, Uchina, Korea Kaskazini, Palestina (Nchi ya), Somalia, Yemen |

## HUKUMU ZA KIFO

Amnesty International ilirekodi hukumu mpya za kifo zipatazo 2,428 mwaka 2023, ambalo ni ongezeko la asilimia 20 kutoka kwa jumla ya hukumu 2,016 ambazo zinajulikana kutolewa 2022. Takwimu za 2023 ndizo zilizokuwa za juu zaidi kurekodiwa tangu 2018, mwaka ambao inajulikana kwamba hukumu mpya 2,531 za kifo zilitolewa. Hata hivyo, tofauti katika upatikanaji wa taarifa kuhusu hukumu za kifo katika baadhi ya nchi hufanya ulinganisho wa takwimu hizi za kimataifa, mwaka hadi mwingine kuwa wenye changamoto.

### MCHORO 2: IDADI YA WATU WALIOHUKUMIWA KIFO DUNIANI 2014-2023




[4] Kama ilivyokuwa miaka ya awali, Amnesty International haikupokea ripoti zozote kuhusu wattu walionyongwa kwa kupigwa mawe 2023.

Amnesty International ilirekodi hukumu mpya za kifo katika nchi 52 mnamo 2023, ambayo ni idadi sawa na iliyorekodiwa mwaka wa 2022. Mahakama katika nchi tano – Bahrain, Commoros, Sudan Kusini, Sudan na Zambia – haijulikani ikiwa ziliwahukumu watu kifo mnamo mwaka wa 2023 ingawa walikuwa wamefanya hivyo 2022. Katika nchi nyingine tano – Belarus, Kameruni, Japan, Moroko/Sahara Magharibi na Zimbabwe – inajulikana kuwa watu walihukumiwa kifo mwaka wa 2023 baada ya sitisho la muda la kuiondoa.

**HUKUMU ZA KIFO ZILIZOREKODIWA ULIMWENGUNI 2023**

Afghanistan (+), Algeria (38+), Bangladesh (248+), Belarus (1), Botswana (2), Kameruni (1+), Uchina (+), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (33+), Misri (590), Ethiopia (3+), Gambia (5), Ghana (10), Guyana (7), India (120). Indonesia (114+), Iran (+), Iraq (138+), Japan (1), Jordan (3+), Kenya (131), Kuwait (9+), Laos (4+), Lebanon (11+), Libya (29+), Malaysia (38+), Maldives (1), Mali (13+), Mauritania (5+), Moroko/ Sahara Magharibi(2+), Myanmar (19+), Niger (8+), Nigeria (246+), Korea Kaskazini(+), Pakistan (102+), Palestina (Nchi ya, 27+), Qatar (8), Saudi Arabia (3+), Singapore (6+), Somalia (31+), Korea Kusini (1), Sri Lanka (40+), Syria (+), Taiwan (3), Tanzania (3+), Thailand (123), Trinidad na Tobago (3), Tunisia (3+), Muungano wa Milki za Kiarabu (4+), Marekani (25), Viet Nam (122+), Yemen (81+), Zimbabwe (3).

Amnesty International ilirekodi ongezeko kubwa la idadi ya hukumu za kifo zinazojulikana kutolewa katika nchi ya Bangladesh (kutoka 169+ mnamo 2022 hadi 248+ mnamo 2023), Misri (kutoka 538 hadi 590), Iraq (kutoka 41+ hadi 138+), Kenya (kutoka 79 hadi 131), Lebanon (kutoka 2+ hadi 11+), Malaysia (kutoka 16+ hadi 38+), Nigeria (kutoka 77+ hadi 246+), Somalia (kutoka 10+ hadi 31+).

Punguo kubwa kiasi la idadi ya hukumu za kifo zilizotolewa lilirekodiwa katika nchi zifuatazo: Algeria (kutoka 54 2022 hadi 38+ 2023), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (kutoka 76+ hadi 33+),Gambia (kutoka 9+ hadi 5+), India (kutoka 165 hadi 120), Kuwait (kutoka 16+ hadi 9+), Myanmar (kutoka 37+ hadi 19+), Saudi Arabia (kutoka 12+ 3+ hadi 3+), Tanzania (kutoka 11 hadi 3+), Tunisia (kutoka 26+ hadi 3+).

Kimataifa, aghalabu watu 27,527 walihukumiwa kifo kufikia mwisho wa 2023.[5]

## PUNGUZO LA ADHABU, MISAMAHA NA KUONDOLEWA HATIA

Amnesty International ilirekodi punguzo la adhabu, au misamaha ya hukumu ya kifo katika nchi 27: Bahrain, Bangladesh, Barbados, Gambia, India, Indonesia, Iraq, Jordan, Kenya, Kuwait, Malaysia, Mali, Moroko/Sahara Magharibi, Myanmar, Niger, Nigeria, Pakistan, Qatar, Somalia, Korea Kusini, Sudan Kusini, Taiwan, Trinidad na Tobago, Muungano wa Milki za Kiarabu, Marekani, Viet Nam, Zambia.[6]

Amnesty International ilirekodi wafungwa 9 walioondolewa hatia baada ya kuhukumiwa kifo katika nchi tatu - Kenya (5), Marekani (3),[7] Zimbabwe (1).[8]

## ADHABU YA KIFO 2023: NI UKIUKAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA

Adhabu ya kifo iliendelea kutumiwa 2023 kwa njia zilizokiuka sheria ya kimataifa na viwango. Baadhi ya mifano ni kama vile:

- Aghalabu watu 8 walinyongwa hadharani nchini Afghanistan (1+) na Iran (7).
- Aghalabu watu watano- nchini Iran - walinyongwa kwa makosa yaliyofanyika wakiwa chini ya miaka 18; Amnesty International waliamini kwamba watu wengine katika kundi hili walibakia kusubiri kunyongwa Iran na Maldives.[9]
- Watu walio na ulemavu wa kiakili walihukumiwa kifo katika nchi kadhaa zikiwemo Japan, Maldives na Marekani.

---

[5] Katika nchi kadhaa ambapo Amnesty International waliamini idadi kubwa ya wafungwa ilikuwa ya wale waliohukumiwa kifo, takwimu hazikuwepo au haingewezekana kamwe kukadiria idadi halisi. Hizi zilikuwa ni pamoja na Misri, Iran, Libya, Korea Kaskazini, Saudi Arabia na Syria.

[6] Punguzo hutokea pale ambapo hukumu ya kifo hubadilishwa kuwa hukumu nyingine nafuu kidogo kama vile kifungo cha maisha, mara nyingi hili likifanywa na mahakama baada ya rufaa lakini pia wakati mwingine kutoka kwa kiongozi wa nchi. Msamaha hutolewa wakati ambapo mtu aliyepatikana na hatia anaondolewa kabisa adhabu zaidi.

[7] Kituo cha Habari kuhusu Hukumu ya Kifo, deathpenaltyinfo.org/policy-issues/innocence-database

[8] Kuondolewa hatia ni pale ambapo baada ya kuhukumiwa na kukamilika kwa rufaa, mtu aliyepatikana na hatia anaondolewa lawama au hatia ya kosa aliloshtakiwa kwalo, na hivyo kuchukuliwa kama mtu asiye na kosa mbele ya jicho la sheria.

[9] Mara nyingi, umri wa mfungwa huwa haujulikani kwa kuwa hakuna ithibati ya umri iliyopo, kama vile cheti cha kusajili mtoto aliyezaliwa. Serikali zinapaswa kutumia njia zinazowezekana kujua umri wa mtu endapo hakuna kinachokuonyesha. Mazoea mazuri katika kutathmini umri wa mtu ni kuangalia alivyokamaa kimwili, kisaikolojia na kijamii. Tathmini kwa msingi huu itumike kwa namna ambayo endapo kuna tashwishi kuhusu kama mtu alikuwa amefikisha miaka 18 au la, achukuliwe kuwa hakuwa amefikisha miaka hiyo wakati kosa lilipofanyika, na hivyo basi ihakikishwe kwamba adhabu ya kifo isitolewe. Mtazamo kama huo unaendana na kanuni kwamba maslahi bora zaidi ya mtoto yaongoze katika kuchukua hatua zote zinazowahusu watoto, kama inavyohitajika katika Ibara ya 3(1) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto.

- Hukumu za kifo zilijulikana kutolewa baada ya kesi ambazo hazikufikia **viwango vya kimataifa vya usawa** wa kesi katika nchi kadhaa, zikiwemo Afghanistan, Bahrain, Bangladesh, Belarus, Uchina, Misri, Iran, Iraq, Malaysia, Myanmar, Korea Kaskazini, Pakistan, Saudi Arabia, Singapore, na Yemen.
- **"Shuhuda"** ambazo pengine zilitolewa kupitia **kuteswa au vitendo vingine vya kikatili** zilitumiwa kutia watu hatiani na kuwahukumu kifo nchini Misri, Iran, Saudi Arabia.
- Hukumu za kifo zilitolewa **bila mshtakiwa kuwepo mahakamani** nchini Banglandeshi na Tunisia.
- **Hukumu za kifo za lazima** zilitolewa Afghanistan, Ghana, Iran, Malaysia, Myanmar, Nigeria, Pakistan, Saudi Arabia, Singapore Trinidad na Tobago.[10]
- **Mahakama za kijeshi** ziliwahukumu kifo raia nchini Myanmar. **Mahakama maalum** zilitoa hukumu za kifo nchini Bangladesh, India, Iran, Pakistan, Saudi Arabia na Yemen.
- Adhabu ya kifo ilitolewa kwa **makosa ambayo hayakuhusu mauaji ya kupangwa** na kwa hivyo hayakufikia viwango vya kuwa "makosa mabaya zaidi" chini ya sheria ya kimataifa:[11]

  **– Makosa yanayohusiana na dawa za kulevya:** Watu walinyongwa kutokana na makosa yanayohusiana na dawa za kulevya nchini Uchina (+),[12] Iran (481), Saudi Arabia (19) na Singapore (5); idadi hiyo ya jumla ya watu 507 ilikuwa asilimia 44 ya jumla ya watu waliorekodiwa kunyongwa duniani. Taarifa kuhusu Viet Nam, ambayo ina uwezekano kwamba waliwanyonga watu kama hao hazikupatikana.

  \- Hukumu mpya za kifo 246 zinajulikana kutolewa katika nchi 10: Bangladesh (1), Uchina (+),[13]Misri (6), Indonesia (99 au 86%), Iran (+), Laos (4 kati ya aghalabu 4, 100%), Malaysia (20 kati ya aghalabu 38, 53%), Singapore (6 kati ya 6, 100%), Sri Lanka (6 kati ya aghalabu 40, 15%) na Viet Nam (100 kati ya aghalabu 122, 82%). Nchini Thailand, kati ya watu 325 waliohukumiwa kifo kufikia mwisho wa 2023, 199 wakiwemo wanawake 26 walipatikana na hatia kutokana na makosa yanayohusiana na dawa za kulevya.

  \- **Makosa ya kiuchumi**, kama vile rushwa: Uchina.

  **– Uasi**: Iran.

  **Mahusiano ya kingono nje ya ndoa baina ya watu wazima waliokubaliana**: Iran.

  **- Utekaji nyara**: Saudi Arabia.

  **- Ubakaji**: Bangladesh, Misri, Iran, Pakistani na Saudi Arabia.

  \- Aina mbalimbali za **"uhaini"**, **"vitendo dhidi ya usalama wa taifa"**, **"ushirikiano"** na watu wa nje, **"ujasusi"**, **"kuhoji sera za viongozi'**, kuhusika katika "**makundi ya wanamgambo na magaidi**", **"uasi wa kivita dhidi ya kiongozi"** na **"makosa mengine dhidi ya nchi"**, yawe yalisababisha kupotea kwa maisha au la: Iran na Saudi Arabia.

[10] Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa imetamka kwamba hukumu za kifo za lazima ambazo huacha mahakama za ndani bila uwezo wa kuamua iwapo wataainisha kosa kama linalostahili kutolewa adhabu ya kifo na ikiwa watoe hukumu ya kifo katika hali fulani za mshtakiwa ni za kiholela " Kamati ya Haki za Binadamu, Maoni ya Jumla Namba. 36 katika Ibara ya 6: Haki ya Kuishi, Hati ya Umoja wa Mataifa CCPR/C/GC/36 [3 Septemba 2019], aya. 37,

[11] Kama ilivyowekwa katika Ibara ya 6 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, Kamati ya Haki za Binadamu, Maoni ya Jumla Namba 36 katika Ibara 6: Haki ya Kuishi, Hati ya Umoja wa Mataifa CCPR/C/GC/36 [3 Septemba 2019], aya. 37.

[12] Wakati wa kuhesabu jumla ya watu duniani na kikanda "+" imetumika kuonyesha wamehesabiwa kama wawili.

[13] Wakati wa kuhesabu jumla ya watu duniani na kikanda "+" imetumika kuonyesha wamehesabiwa kama wawili.

# AFRIKA KUSINI MWA SAHARA

# MIENENDO YA KIKANDA


- Kulikuwa na ongezeko kubwa na la haraka katika matumizi ya adhabu ya kifo kwenye kanda hii; idadi iliyorekodiwa ya watu ambao walinyongwa iliongezeka zaidi ya mara tatu na hukumu za kifo zilizorekodiwa ziliongezeka pakubwa kwa asilimia 66.
- Somalia ndiyo nchi ya pekee inayojulikana kwamba iliwanyonga watu.
- Hukumu za kifo zilirekodiwa katika nchi 14, ambalo ni punguo la nchi 2 ikilinganishwa na mwaka 2022.
- Nchi nne zilichukua hatua chanya za kuunda sheria ya kukomesha adhabu ya kifo.

| NCHI | IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA 2023 | HUKUMU ZA KIFO ZILIZOREKODIWA 2023 | WATU WANAOJULIKANA KUHUKUMIWA KIFO KUFIKIA MWISHO WA 2023 |
|---|---|---|---|
| BOTSWANA | 0 | 2 | 15+ |
| BURKINA FASO | 0 | 0 | 0 |
| KAMERUNI | 0 | 1+ | + |
| COMOROS | 0 | 0 | + |
| JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO | 0 | 33+ | + |
| EQUATORIAL GUINEA | 0 | 0 | 0 |
| ERITREA | 0 | 0 | |
| ESWATINI | 0 | 0 | 1 |
| ETHIOPIA | 0 | 3+ | + |
| GAMBIA | 0 | 5 | 18 |
| GHANA | 0 | 10 | 180 |
| KENYA | 0 | 131 | 120 |
| LESOTHO | 0 | 0 | 0 |
| LIBERIA | 0 | 0 | 15+ |
| MALAWI | 0 | 0 | + |
| MALI | 0 | 13+ | + |
| MAURITANIA | 0 | 5+ | 170+ |
| NIGER | 0 | 8+ | 8+ |
| NIGERIA | 0 | 246+ | 3413+ |
| SOMALIA | 38+ | 31+ | + |
| SUDAN KUSINI | 0 | 0 | + |
| SUDAN | 0 | 0 | + |

| NCHI | IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA 2023 | HUKUMU ZA KIFO ZILIZOREKODIWA 2023 | WATU WANAOJULIKANA KUHUKUMIWA KIFO KUFIKIA MWISHO WA 2023 |
|---|---|---|---|
| TANZANIA | 0 | 3+ | 691 |
| UGANDA | 0 | 0 | + |

| NCHI | IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA 2023 | HUKUMU ZA KIFO ZILIZOREKODIWA 2023 | WATU WANAOJULIKANA KUHUKUMIWA KIFO KUFIKIA MWISHO WA 2023 |
|---|---|---|---|
| ZAMBIA | 0 | 0 | |
| ZIMBABWE | 0 | 3 | 59+ |

## MCHORO 7: IDADI ILIYOREKODIWA YA WATU WALIONYONGWA NA WALE WALIOHUKUMIWA KIFO AFRIKA KUSINI MWA SAHARA 2014-2023




Mnamo mwaka 2023, Afrika Kusini mwa Sahara ilirudisha nyuma ufanisi uliokuwa umepatikana dhidi ya adhabu ya kifo mwaka uliotangulia.  Kulikuwa na ongezeko la idadi iliyorekodiwa ya watu ambao walihukumiwa kifo na kunyongwa mnamo mwaka 2023 na hakuna nchi iliyokomesha adhabu ya kifo tangu mwaka 2022.

Idadi iliyorekodiwa ya watu walionyongwa katika kanda hii iliongezeka mara tatu kutoka 11 mwaka 2022 hadi 38 mwaka 2023, ingawa watu hawa wote walirekodiwa katika nchi moja – Somalia – ambapo ikilinganiswa na 2022, watu walionyongwa waliongezeka kwa idadi kubwa kutoka 6 hadi 38. Licha ya nchi zinazowanyonga watu kupungua - kutoka mbili mwaka wa 2022 hadi moja mnamo 2023 – idadi iliyorekodiwa ya watu 38 walionyongwa ndiyo iliyokuwa ya juu zaidi kurekodiwa katika kanda hii tangu 2015.

Hukumu za kifo zilizorekodiwa ziliongezeka kwa asilimia 66 kutoka 298 mnamo 2022 hadi 494 mnamo 2023. Amnesty International ilirekodi hukumu za kifo katika nchi 14, nchi mbili chini ya zile zilizorekodiwa mwaka uliotangulia. Ikilinganishwa na 2022, kulikuwa na ongezeko la hukumu za kifo zilizorekodiwa katika nchi zifuatazo: Kameruni (0 hadi 1); Ethiopia (2 hadi 3); Ghana (7 hadi 10); Kenya (79 hadi 131); Mali (8 hadi 13); Niger (4 hadi 8); Nigeria (77 hadi 246); Somalia (10 hadi 31); na Zimbabwe (0 hadi 3).

Hakuna nchi iliyokomesha adhabu ya kifo katika kanda hii mwaka wa 2023 ingawa mabunge ya nchi nne yalichukua hatua chanya kuelekea ukomeshaji wake. Mnamo Julai, Bunge la **Ghana** lilipiga kura kuunga mkono miswada miwili ambayo iliondoa adhabu ya kifo kutoka kwenye Sheria ya Jinai na Makosa Mengineyo ya 1960, na Sheria ya Majeshi ya 1962. Mnamo Novemba, Rais Nana Akufo-Addo aliliandikia Bunge la Ghana kusema kwamba amekataa kutia sahihi Mswada wa Sheria ya Makosa ya Jinai (Marekebisho) (Namba 2) ya 2023 na Mswada wa Sheria ya Majeshi (Marekebisho) ya 2023 ("miswada"). Rais Akufo-Addo aliliambia Bunge kwamba alikataa kutia sahihi miswada hiyo kwa sababu ilikuwa imeletwa Bungeni kama miswada ya watu binafsi, kinyume na Ibara ya 108 ya Katiba ya Ghana ambayo huhitaji miswada ya Sheria muhimu kama hiyo iletwe bungeni na/au kwa niaba ya Rais.[14] Kufikia mwisho wa mwaka, Miswada hiyo haikuwa imefanywa kuwa sheria. Mtu wa mwisho anayejulikana kunyongwa nchini Ghana ilikuwa mwaka 1993.

Nchini **Kenya**, miswada minne ya kukomesha adhabu ya kifo ilipelekwa Bungeni kati ya Agosti na Septemba. Kwanza, Mswada wa Kudumisha Usalama wa Umma (Marekebisho) wa 2023 uliopelekwa Bungeni mnamo Agosti unataka kukomeshwa kwa adhabu ya kifo kwa makosa yanayohusiana na udumishaji wa usalama wa umma. Pili, Mswada wa Usaidizi wa Kisheria (Marekebisho) wa 2023, ulioletwa Bungeni unataka kufutwa kwa marejeleo ya adhabu ya kifo katika Sheria ya Usaidizi wa Kisheria (Namba. 6 ya 2016). Tatu, Mswada wa Magereza (Marekebisho) wa 2023 uliofikishwa Bungeni mnamo Septemba unataka kufanyiwa marekebisho Sheria ya Magereza CAP 90, Sheria za Kenya ili kukomesha adhabu ya kifo na njia za kuitekeleza. Tatu, Mswada wa Kanuni ya Adhabu (Marekebisho) wa 2023 uliopelekwa Bungeni mnamo Septemba unataka marekebisho yafanyiwe Sheria ya Kanuni za Adhabu CAP 63 Sheria za Kenya ili kukomesha adhabu ya kifo. Mtu wa mwisho anayejulikana kunyongwa nchini Kenya ilikuwa mwaka 1987.


Nchini **Zimbabwe**, mswada wa kukomesha adhabu ya kifo nchini humo ulichapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali mnamo Disemba.[15] Mswada huu unalenga kukataza kutolewa kwa hukumu za kifo na mahakama; kuipa nguvu Mahakama ya Upeo kuweza kubadilisha adhabu ya kifo na hukumu nyingine inayofaa wakati inaposikiliza rufaa dhidi ya adhabu ya kifo; kumkataza mtu yeyote kutekeleza adhabu ya kifo ambayo mahakama ilikuwa imetoa hapo awali; na kuondoa adhabu ya kifo kutoka kwenye vipengee vya sheria zilizopo. Mtu wa mwisho anayejulikana kunyongwa nchini Zimbabwe ilikuwa mwaka wa 2005.

Nchini **Liberia**, mswada wa kukomesha adhabu ya kifo nchini humo ulikuwa unasubiri kujadiliwa katika Bunge la Wawakilishi mwishoni mwa mwaka. Mswada huo ulikuwa umepitishwa na wabunge wote wa Seneti mnamo 2022. Mtu wa mwisho anayejulikana kunyongwa nchini Liberia ilikuwa mwaka 2000.


Katika nchi kadhaa kwenye kanda hii, aghalabu watu 1,026 walibadilishiwa adhabu zao na wengine 83 wakasamehewa mnamo 2023, na aghalabu 5 wakaondolewa hatia. Kubadilishiwa adhabu na nyingine ndogo kulifanyika nchini Gambia (1); Kenya (606); Niger (8); Nigeria (20); Somalia (1); na Zambia (390). Mamlaka zilitoa msamaha katika nchi zifuatazo: Gambia (9); Mali (3); Nigeria (35); na Sudan Kusini (36). Nchini Kenya, watu watano ambao walikuwa wamehukumiwa kifo waliondolewa hatia na mahakama.

[14] Kutiwa sahihi kwa Miswada hiyo kuwa sheria ingekuwa hatua muhimu sana kuelekea kukomeshwa kwa adhabu ya kifo nchini Ghana. Hata hivyo, zaidi ya Miswada hii kuwa sheria, kwa kuwa Ibara ya 3(3) ya Katiba ya Ghana ya 1991 imeweka adhabu ya kifo kuwa adhabu kwa kosa la uhaini, kuondolewa kwa kipengee cha adhabu ya kifo kwenye Katiba kutahitajika ili Ghana iwe imekomesha adhabu ya kifo kwa makosa yote.
[15] "Bill to abolish the death penalty gazetted", *The Herald*, 15 December 2023, https://www.herald.co.zw/bill-to-abolish-death-penalty-gazetted/

## MCHORO 8: IDADI YA NCHI ZINAZOFAHAMIKA KWAMBA ZILIWANYONGA WATU AFRIKA KUSINI MWA SAHARA 2014-2023




## MCHORO 9: WALIOPUNGUZIWA ADHABU YA KIFO NA MISAMAHA ILIYOPEANWA AFRIKA KUSINI MWA SAHARA MWAKA 2023



## AMNESTY INTERNATIONAL NI VUGUVUGU LA KIMATAIFA LA KUTETEA HAKI ZA BINADAMU.

## UONEVU UNAPOFANYWA KWA MTU MMOJA, HILO NI SUALA LINALOTUGUSA SISI SOTE.


WASILIANA NASI:

info@amnesty.org

+44 (0)20 7413 5500


JIUNGE KWENYE MAZUNGUMZO

www.facebook.com/AmnestyGlobal

@Amnesty

# HUKUMU ZA KIFO NA WATU WALIONYONGWA 2023

Ufuatiliaji wa Amnesty International wa matumizi ya adhabu ya kifo duniani ulibaini watu 1,153 wanaofahamika kuwa walinyongwa mwaka 2023, ambalo ni ongezeko la asilimia 31 kutoka 883 mwaka 2022. Hata hivyo nchi zinazowanyonga watu zilipungua kwa kiwango kikubwa kutoka 20 mwaka 2022 hadi 16 mwaka 2023.

Ongezeko hili kubwa la visa vinavyofahamika vya watu walionyongwa duniani lilitokana na ongezeko la visa vilivyorekodiwa nchini Irani, ambapo idadi iliongezeka kwa asilimia 48 kutoka 576 mwaka 2022 hadi 853 mwaka 2023. Hii ni sawa na takribani asilimia 74 ya watu wote walionyongwa duniani. Idadi iliyorekodiwa ya watu walionyongwa nchini Saudi Arabia ilipungua kwa asilimia 12, kutoka 196 mwaka 2022 hadi 172 mwaka 2023.

Ikilinganishwa na mwaka 2022, ongezeko kubwa la idadi ya watu walionyongwa lilirekodiwa nchini Iran, Somalia, Yemen na Marekani, huku idadi hiyo ikiripotiwa kupungua nchini Misri, Saudi Arabia na Singapore. Siri serikalini na vikwazo vinginevyo nchini Uchina, Korea Kaskazini  na Viet Nam, miongoni mwa nchi zingine ni mambo yaliyozuia kufanyika kwa tathmini sahihi ya matumizi ya adhabu ya kifo.

Ijapokuwa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu inakataza matumizi ya hukumu ya kifo kwa uhalifu au makosa ambayo hayajafikia viwango vya kuwa “uhalifu mbaya zaidi” (uhalifu unaohusu mauaji ya kimaksudi), katika aghalabu nchi tano - Uchina, Iran, Kuwait, Saudi Arabia na Singapore ziliwanyonga watu kwa makosa yanayohusiana na dawa za kulevya. Jumla ya watu 508 walirekodiwa kunyongwa, hilo likiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 56 ikilinganishwa na idadi iliyorekodiwa mwaka 2022. Nchini Iran, makosa yanayohusiana na dawa za kulevya yaliwakilisha zaidi ya asilimia 56 (watu 481) ya jumla ya watu walionyongwa.

Hata hivyo, ulimwengu ulipiga hatua katika kukomesha adhabu ya kifo. Nchini Pakistan na Malaysia, adhabu ya kifo kwa makosa yanayohusiana na dawa za kulevya na adhabu ya kifo ya lazima zilifutwa mtawalia. Katika kanda ya Afrika Kusini mwa Sahara, mabunge ya nchi nne – Ghana, Kenya, Liberia na Zimbabwe – yalichukua hatua chanya kuelekea ukomeshaji wa adhabu ya kifo.

**FAHIRISI: ACT 50/7952/2024**
**MAI 2024**



AMNESTY INTERNATIONAL